# PROPAGANDA

## NIUENI MKITAKA, UKWELI WOTE NITASEMA

JOHN WISSE

DAROHN
TANZANIA-KENYA-UGANDA-SUDANI-RWANDA

Darohn 5 Press Tanzania Ltd,
P.O.BOX 21345,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Darohn 5 Press Uganda Ltd,
P.O.BOX 32453,
JINJA ROAD-BC657,
UGANDA.

Darohn 5 Press Kenya Ltd,
Mombasa Road,
P.O.BOX 21345,
NAIROBI,
KENYA.

ISBN: 978-9987-9836-0-2 3
*Riwaya*

© 2021, Darohn 5 Press

Chapa ya kwanza, Mei 2022

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kupiga chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa Darohn 5 Press Tanzania Ltd.

Wapiga chapa ni
**Info tech, Malaysia**

# RAI YA MTUNZI / MWANDISHI

*"Hofu ni chanzo cha mambo mengi kuharibika..ukiishinda hofu utakuwa shujaa hata wakati wako wa kufa."*

---

Mpendwa msomaji, hii ni hadithi ya kubuni ambayo visa na mikasa iliyoumbwa yaweza kufanana sana na hali halisi ya maisha waishiyo binadamu wa sasa. Kwa kufanya hivyo ni kutaka kusawiri na kuakisi ukweli wa mambo ambayo fasihi ya maandishi hulenga, hasa kuifikishia ujumbe hadhira kwa mujibu wa mazingira yake.

Kwa yeyote asomaye kitabu hiki, itoshe kusema kuwa, falsafa ya mwandishi haiwezi kuwa falsafa yako msomaji kwa kuyatilia maanani yote yaliyoandikwa, kwa maana ni hiari ya kila mmoja aliye huru kuamua kufanya jambo lolote kwa mustakabali wa maisha yake, ila tu asiwe anavunja sheria.

Aidha, nchi ya Tuvumiliane ni ya kubuni, ambako visa hivi vimetokea inaweza kuwa nchi yo yote barani Afrika, hata nje ya Afrika ambako visa na mikasa hii vyaweza kutokea.

Kwa msisitizo zaidi, majina ya wahusika katika riwaya hii ni ya kubuni tu, na endapo yatafanana ama kurandana na watu halisi waishio duniani hata ahera, basi itoshe kuwa ni bahati tu na dhahania iliyolenga kuleta msisimko wa kifasihi.

Hivyo basi, nawasihi wasomaji wangu kusoma mkasa huu wa kipelelezi kwa makini, tena wasisite kusoma mfululizo wa simulizi za mpelelezi niliyemuumba, bwana Raymond Masele, a.k.a Chato. Kila mwezi kitatoka kitabu kimoja chenye kisa kinachojitosheleza kwa bei rafiki kwa msomaji, kisichochosha kwa urefu, lakini kilichojaa taharuki. Usikose uhondo huu unaokujia kwa uhakika zaidi, kwa bei nafuu.

Niwe shuhuda kwenu kuwa, Korona ipo. Kumbuka kuchukua tahadhari-jikinge na wakinge wengine pia. Chanjo ni hiari yako, lakini ni muhimu kwa mustakabali wa afya yako endapo utaona inafaa!

Wasalaam,

**J.W.**

## Dondoo

Wakati simu yangu ya mkononi inaita, nilikuwa namalizia zoezi la kumuua mtu. Nilimvuta na kumtelekeza kichakani ndipo nikaipokea simu ile.

"Chato umefanya kosa—hukupaswa kufanya hivyo," alisema Frank.

"Kosa gani—la ki usalama?" nikauliza nikiwa bado na maswali mengi kichwani. Nikaangaza macho huku na kule kama Frank alikuwa karibu na mahali nilikuwa.

"Kumuua mtu huyo, huku unajua kabisa hakustahili kuuawa mapema namna hii. Mbaya zaidi sehemu uliyomuulia na unamficha hadi sasa maadui wamekuzingira. Nawe utauawa hivi punde," akasema Frank.

Niligeuka kila upande kutazama katika eneo lile la vilima. Nikaona pako shwari lakini bado mwili ulijaa sisimko la kuwa kuna watu wananivizia. Nilipotaka

kutoroka eneo hilo, niliona kundi kubwa la watu waliovaa nguo nyeusi na wameficha nyuso zao. Mmoja wao akatoa amri, “Weka silaha chini—lala kifudifudi. Ukikaidi tutakuua mara moja!”

Kwa jeuri nikajibu, “Niueni mkitaka!”

Mmoja akanishona risasi kwenye mkono uliokuwa na bastola hata nikaiangusha. Nikapigwa na kitako cha bunduki kichwani kilichonifanya nianguke na kupoteza fahamu palepale…….

# 1

Nilikuwa katikati ya safari yangu nikitokea Jiji la Mawe nikielekea Jiji la Joto katika ukanda wa Afrika Mashariki. Nilikuwa nimemwacha mtoto wangu shuleni alikokuwa akisoma huko Nyanza baada ya shule kufunguliwa.

Nikiwa katika basi la Kampuni ya *Lake Connection,* usingizi ulianza kunichukua taratibu kutokana na uchovu wa safari iliyochukua masaa takribani saba nikiwa katika kiti cha basi. Nikiwa sijatopea usingizini bado, ningali natafakari, kwa mbali nilisikia mtingishiko wa simu yangu katika mfuko wa ndani wa koti la suti

nililokuwa nimevaa. Nikautuma mkono taratibu na kuichomoa simu huku nafumbua macho ili nitazame na kuhakiki kuwa ni nani alikuwa ananipigia.

Katika kioo cha simu yangu ndogo nikaliona jina la mkuu wa kitengo cha upelelezi kinachoitwa Silent Detectives (SD). Hiki kilikuwa ni kitengo cha siri nilichokuwa nakifanyia kazi takribani miaka minane mfululizo. Jukumu tulilopewa ni kuhakikisha tunakuwa jicho la kikosi cha Usalama wa Taifa nje ya mfumo rasmi uliowekwa na serikali. Ulikuwa wajibu wetu kuhakikisha kuwa, watu wa usalama wa taifa na vyombo vyote vya ulinzi vilifanya kazi sawasawa kwa maslahi ya taifa. Na kama kulikuwa na walakini, basi ulikuwa wajibu wetu kuingilia kati na kuweka mambo sawa.

Baada ya kuliona jina la mkuu wangu wa kitengo cha Silent Detectives (S.D) niliminya kitufe cha kijani ili nizungumze naye.

“Mkuu!” Nikaongea kwa sauti kakamavu.

“Umefika wapi, Raymond?” Kachero Frank akaniuliza.

“Katikati ya nchi, mkuu!”

“Gari uliyopanda ni ndege. Saa saba hii upo Katikati ya nchi!”

“Mwendo wa kawaida tu mkuu—si unajua siku hizi hata barabara ni nzuri tofauti na zamani—lami kila kona sasa, kwanini mabasi yasitembee kwa mwendo kasi kama huu? Binafsi naona ni kawaida.”

“Huogopi ajali, Ray!”

“Kama siogopi risasi mkuu wangu, iweje sasa niogope ajali ambayo hata sijui wakati itatokea?”

Tulicheka kila mmoja na upande wake.

“Basi, hebu achana na hilo. Nimekupigia simu kwa jambo maalumu.”

Nikashtuka. Maana namjua Kachero Frank vema—akisema kuna jambo maalumu basi ukae chonjo kukabiliana na mazito.

“Lipi mkuu?”

Kabla hajanijibu nilisikia sauti kwa mbali ambayo sikuielewa ikinong’ona kama kumwelekeza Kachero Frank cha kuzungumza. Kwakuwa nilisikia ni sauti yake, nikapuuza na kujua kuwa huenda wakati ananipigia alikuwa na msaidizi wake akifanya mambo mawili kwa wakati mmoja.

“Nimepokea simu kutoka Hazina ya vito vya thamani. Kuna shehena ya dhahabu imetoweka katika mazingira ya kutatanisha. Nimejaribu kufuatilia kwa ukaribu na inaonesha mpango huu umesukwa na watu muhimu ndani ya serikali—na kuna kila dalili kuwa baadhi ya watumishi ndani ya usalama wa taifa wanahusika, na wapo nyuma ya mpango huu.”

Nikavuta pumzi ndefu kisha kuzishusha ndipo nikabaki kumsikiliza Kachero Frank.

Bado niliendelea kusikia sauti nisizozielewa mantiki yake.

“Chato, umelala ama nini—mbona kimya?”

“Nipo natafakari, mkuu.”

“Huu si muda wa kutafakari, yafaa kuchukua hatua haraka. Hapo Katikati ya nchi shuka mahali popote ulipo. Tiketi ya ndege ipo tayari. Kwa maana hiyo nenda uwanja wa ndege wa Kivumbini utakuta ujumbe wako pale mapokezi.”

“Nikamuone nani, mkuu.”

“Muone namba 218-PJ!”

“Nimeshakuelewa.”

Alikata simu.

Kwa hali ile ilinipasa kushuka haraka kwani basi lilikuwa halijatoka katika maegesho yaliyopo katika kituo kile cha mafuta, ambapo wasafiri walikuwa wakipata huduma mbalimbali kama *‘kuchimba dawa’* na kujipatia vyakula na

vinywaji. Zilikuwa zimesalia dakika kama tatu tu kati ya kumi ili basi liondoke. Kwa udharura niliofahamishwa sasa ikalazimu nichomoe kibegi changu kidogo kilichokuwa katika rafu za basi lile na kushuka bila hata kuaga yeyote. Wakati natoka ndipo nikakutana na Kondakta mlangoni. Akaniambia, “Usiende mbali—tunatoka sasa hivi.”

“Safari yangu imeishia hapa. Nimepata dharura!”

Kondakta badala ya kuuliza dharura niliyoipata ilihusu nini—akatabasamu. Sikuona ajabu kwani tayari nilijua alikuwa kafurahi kushuka kwangu kabla ya kufika mwisho wa safari ili apate kuuza siti kwa mara ya pili tofauti na ilivyokuwa. Kwa vielelezo alivyokuwa navyo tiketi yangu ilisomeka kuwa safari yangu ilikuwa iishie jijini Jiji la Joto kutokea Jiji la Mawe, na ningeshukia pale Mtaa za Giza. Sasa kwake ikawa sherehe kwa maana alikuwa kapata

fursa ya kuuza kiti changu na fedha ni halali yake wala si ya mwajiri wake.

Nikatoka eneo la kituo kile cha mafuta kwa ujasiri na kuchepuka hadi kando ambapo kulikuwa na pikipiki. Macho yangu wakati nawaelekea dereva wa bodaboda zile yalikuwa yakimkagua mmoja baada ya mwingine ili nijue afaaye kunichukua kutokea hapo.

Kuna mmoja kati ya wengi niliona atanifaa. Alikuwa kavaa vizuri viatu vya kufunika vilivyo vya ngozi na vigumu. Alikuwa na kofia ngumu mbili za ziada na pikipiki yake ilikuwa bado mpya.

Nikaita, "Wewe macho manne!"

Akanitazama. "..twende!"

Kwakuwa kati ya wote aliyevaa miwani alikuwa ni mmoja, aliwasha pikipiki yake haraka na kunisogelea. Niliketi kwa nyuma na kumruhusu kutoka mahali hapo hata bila kumwambia niendako. Kwa uzoefu wake pengine sikujua ni kwanini, ila nikajua

alikuwa mbobevu wa saikolojia ya wasafiri na huenda alijua nielekeako kuwa ni katikati ya jiji la Katikati ya nchi. Akashika njia iendayo mjini kati na hapo ndipo nikamwambia, "Nipeleke Kivumbini ."

"Kivumbini shule ya sekondari?" Akaniuliza.

"Uwanja wa ndege!" nikamjuza.

"Bei ya huko unaijua?"

"Endesha tufike, pesa si tatizo…nitakulipa pesa inayotosha safari yote."

Dereva wa bodaboda yule alikuwa jeuri kiasi cha kufunga breki. Akataka kwanza tukubaliane kiasi cha kumlipa. Niliafiki bei aliyonitajia japo kwa shingo upande. Akataka nimlipe shilingi 15,000/= jambo ambalo niliona ni la kawaida kwa mazingira ya uharaka niliyokuwa nayo wakati ule.

Tulipanda na kushuka katika barabara akiwa kaichochea pikipiki ikienda kwa

mwendo mkali ili niwahi. Aliponifikisha karibu na uwanja wa ndege sikutaka aendelee kuwa nami. Nikamtaka afunge breki ili anishushe kabla sijafika eneo la uwanja wa ndege.

"Nikajua nakupeleka kwenda kupanda ndege?" akaniuliza.

"Hapana. Nataka nimpigie simu mwenyeji wangu, anakaa maeneo haya upande wa pili na uwanja." Nikamdanganya.

Nilipompatia pesa yake kutoka katika pochi yangu, nikaona anakenua meno kama ngiri. Akanishukuru na kuiwasha tena pikipiki yake ili aondoke. Alipoondoka nikashukuru kwani nilipata wasaa wa kuvuta hewa safi tofauti na harufu kali iliyonichukiza; harufu iliyokuwa imeufunika mwili wake ilikuwa mbaya. Ukweli dereva yule alikuwa mvuta sigara asiyejali kwani hata wakati ule hakuwa anavuta bado harufu ya sigara ilininyanyasa,

achilia mbali bufuu kali la majasho alilokuwa nalo.

Nilimsindikiza kwa macho kisha nikavuka upande wa pili wa barabara na kuanza kutembea nikielekea uliko uwanja wa ndege. Wakati naushika mlango wa kuingia eneo la mapokezi, nikapokea simu tena.

"Bila shaka naongea na Raymond, alimaarufu Chato!"

Nikasita kuijibu moja kwa moja, badala yake nikaichunguza ile namba iliyonipigia kama naifahamu au la. Ilikuwa namba ngeni.

"Wewe nani?" Nilihoji.

"Utajua baada ya kukueleza nia ya kukupigia simu hii."

Nikashtuka tena.

Sauti ya aliyenipigia ni ya kike, papohapo katika maongezi nikasikia sauti ya mtoto akilia kama anateswa. Moyo wangu ukaweweseka sana.

“Bwana Chato—usitake kulijua jina langu. Lakini kwa faida ya masikio yako, naitwa Nora…”

“Unataka nini, Nora?”

“Nataka urudi Jijini Mwanza haraka. Kuna kazi ya dharura unapaswa kuja kuifanikisha.”

Maneno ya Nora yakanishangaza. Ati nirudi nilikotoka. Si upuuzi huo! Kwanza sikuwa namfahamu Nora, na wala sijawahi kujuana naye kabla. Nikastaajabu tena na tena kuipokea simu kutoka kwake. Si kupokea simu tu, nikashangaa ni wapi alipata namba yangu ile muhimu ambayo ni watu wachache tu tu wa usalama ndio waliifahamu, hasa wakuu wa kitengo cha upelelezi.

“Kazi?” Nikauliza.

“Ndiyo—kazi ya muhimu sana.”

“Muhimu bila kunieleza ni kazi gani?”

“Utaijua ukifika.”

“Kwakweli haiwezekani. Kama huwezi kuniambia hiyo kazi, hata sikuelewi.”

Mwanamke yule nikasikia amenyang’anywa simu.

“Sikia Chato—hatukuombi kuja Jiji Mwanza, ila lazima uje. Tunakuhitaji kwa haraka.”

“Ombi au lazima?” nikauliza utafikiri sijaelewa maneno yake. Mwanaume yule akacheka kwa dharau. Sauti yake ilikuwa nzito kiasi lakini yenye wingi wa mikwaruzo.

“Lazima—siyo ombi! Ukikaidi utajutia maamuzi yako.”

Maneno yale yakanikasirisha sana. Nikakata simu nikidhani kuna mchezo nilikuwa nachezewa, tena mchezo wa kipuuzi.

Sekunde ileile nikaona tena simu inaita. Nikasita kuingia pale mapokezi na badala yake nikasimama kando ya mlango na

kuipokea simu ile. Nilipoipokea tu, nikapata ujumbe, “Tazama nyuma yako, upande wa kuondokea wasafiri!”

Niligeuka kutazama mahali kule.

Nilichokiona nilibaki mdomo wazi. Kulikuwa na wanaume wawili wakinichekea utadhani waliniona bwege kweli katika maisha yangu. Walivaa suti nadhifu za rangi nyeusi na miwani. Nilipowaona nilikata simu nikawatazama na kuwaonesha alama ya dole kuwa niliwatukana kwa dharau. Nikausukuma mlango wa mapokezi na kuingia ndani.

Katika mapokezi nikajaribu kuchunguza mtu ambaye alikuwa na ujumbe wangu. Kwa kawaida, namba ya mtu niliyepewa kama ndiye mwenye taarifa zangu za safari alikuwa mwanamke, sasa nikastaajabu kuona napokelewa na mwanaume. Akaniambia, “Wale pale ndio wenye vielelezo vya safari yako!”

Nikaingiwa mashaka! *Yaani wale wanaume wawili waliojaa jeuri ndio wenye vielelezo?* Nilichojiuliza ni kwamba wale walikuwa akina nani? Na walinifahamu vipi hadi wakawa katika mazingira yale? Wakati natafakari, wanaume wale waliokuwa katika lango la kuondokea wasafiri walianza kupiga hatua kunifuata nilipo. Nikawa na hisia mchanganyiko—ile ya hofu na nyingine ya stara. Nikausogeza mkono wangu nikapapasa mahali nilificha bastola yangu ili likitokea jambo lolote la kunifedhehesha basi niweze kurejesha heshima yangu. Ajaye na aje, iwe kwa heri ama shari, nilikuwa tayari.

# 2

Wakati wanaume wale wanakuja mahali nilikuwa, nikiwa katika chumba cha mapokezi, mwanaume niliyemuuliza na akanielekeza kuwa wale ndio walikuwa na vielelezo vyangu vya safari alinipatia barakoa.

“Vaa barakoa hii kabla hujapatiwa huduma zaidi. Haturuhusu msafiri yeyote kuvuka hapa na kuingia kwenye ndege bila kuwa na barakoa.”

Niliafiki kwa kuwa ulikuwa utaratibu wa dharura ambao ulikuwa umeanza kuzoeleka. Nikaipokea barakoa niliyokuwa nimepatiwa. Niliigeuzageuza kuikagua

lakini mwishowe nikaivaa baada ya wale wanaume wawili nao kuwa wamevaa barakoa zao kabla hawajaingia chumba cha mapokezi japo niliwaona kupitia katika kioo.

Wanaume wale walipoingia mmoja alielekea kwenye kiti ambacho kando kulikuwa na meza ndogo. Akavuta saraka (droo) na kutoa bahasha ya kaki.

"Bwana Chato, unaonekana unapenda sana shari. Kwanini ulikuwa unatuonyeshea ishara ya ya matusi vile?"

"Ishara gani?" Nikauliza kwa sauti iliyojaa utulivu.

"Hicho kidole chako cha kati kutunyanyulia, ulimaanisha nini?"

Nikanyamaza.

"*Anyways!* Hii kwenye bahasha ni tiketi yako ya ndege. Bila shaka Kachero Frank alikujuza kuwa utachukua tiketi hapa!"

"Naam!" Nilijibu.

Watu wale watatu wakawa wanatazamana. Kilichonitokea ni kuhisi kukereketwa puani baada ya kuwa nimekaa na barakoa ile kwa muda kiasi. Nikahisi kupiga chafya na wakati huohuo nikahisi macho yanakuwa mazito kama mwenye kutaka kulala. Nikajaribu kujizuia nisilale lakini nikaona usingizi unanifuata kwa kasi. Baada ya sekunde kadhaa nikajikuta nazidiwa. Nilipoteza fahamu na sikujua walichokuwa wamenifanyia japo nilihisi kuna mchezo umefanywa lakini nilikuwa nimechelewa kujitetea.

*****

Lilikuwa jambo gumu kukubaliana na ukweli kuwa tayari nilitekwa na genge la wahalifu, lilelile ambalo nilihisi kuwa ndilo lilikuwa limehusika na wizi wa shehena ya dhahabu kutoka hazina kama alivyonidokeza Kachero Frank.

Nora, mwanamke aliyenipigia simu alikuwa mbele yangu sambamba na mwanaume mwingine ambaye umbile lake lilikuwa kubwa. Nikijaribu kumtazama Nora, ni mwanamke mrembo, umbile lake la kuvutia sana, ila kasoro yake ilikuwa imebebwa kichwani kwake. Alikuwa na macho makubwa yanayobishana kila akitazama. Isitoshe upande wa jicho la kulia hakuwa na nyusi ila kulikuwa na kovu kubwa lililouvuruga uzuri wake. Mbaya zaidi, mdomoni hakuwa na meno karibu nusu yote.

Nilipokuwa nimefungwa akanijia mwanaume yule mwenye misuli minene. Akasimama kwa kando na kuanza kunitazama kwa dharau.

“Bwana Chato, nisamehe kwa namna umefikishwa hapa. Hakika ulikuwa si uungwana kukuleta hapa kama mhalifu. Imetokea hivyo kwa sababu tunakujua wewe ni mkaidi, kisirani na mtu hatari.”

Sikujibu.

“Eeh! Nadhani uliposhuka pale sheli kutoka kwenye basi hukujua kama simu uliyoipokea haikuwa na ujumbe sahihi. Aliyekupigia simu kweli ni mkuu wako wa kitengo ambaye hadi sasa tunamshikilia. Mbali na mkuu wako, tunashikilia pia mtoto wako wa kiume uliyekuwa umempeleka shuleni pale Nyanza International Academy. Na kama huamini, tazama hii…”

Akaniwashia simu na kunionesha video. Nikaona jinsi mwanangu Allen alishikiliwa na kuegeshewa kisu shingoni. Mtoto akalia akisema nikubaliane na sharti lolote watakalolisema ili asipoteze maisha. Vilevile nilioneshwa Kachero Frank, ambaye ni mkuu wangu wa kitengo cha Silent Detectives (S.D) jinsi alikuwa kapatiwa kipigo cha haja, pia jinsi alikuwa akitoa ishara iliyonitia moyo kuwa alikuwa tayari kutetea maisha na kazi yake kwa namna yoyote. Ishara ile wakati video inarekodiwa

ilikuwa na mafumbo kwa namna tulifundishwa. Jinsi alikuwa akiumba maneno kwa ishara ya mikono yake kulinifanya kujua kuwa, Frank angeweza kujitetea kutokana na mazingira yale kuwa na kasoro za kijasusi ambayo kwake ilikuwa faida.

Mwanaume yule akanisogelea.

“Chato, ninachotaka kutoka kwako ni kimoja tu.”

“Nini? Kama dhahabu mmechukua, unachotaka tena ni nini?”

“Si hivyo Chato. Taarifa kuwa dhahabu imeibiwa ni propaganda tu ili uitikie mapema wito tulioutoa. Tunakujua wewe na hao jamaa zako jinsi huwa mpo makini kuitikia wito wa kuzima hujuma kubwa kama hizo ndani ya kijiwe chenu ili mjipatie sifa dhidi yetu. Ukweli ni kwamba hakuna kulikoibiwa dhahabu wala hakuna dhahabu iliyoibiwa.”

“Sasa ni nini unataka?”

“Tumetumwa!”

“Nani kawatuma?”

“Hupaswi kumjua!”

“Kama sipaswi kumjua, yanini kuniweka hapa?”

“Nisikilize Chato. Kuna jambo moja unapaswa kulijua.”

“Lipi?”

“Kukamatwa kwako pamoja na mkuu wako wa kitengo kunafuatia msimamo wenu hasi, wa kupinga hatua zinazochukuliwa na serikali dhidi ya ugonjwa wa Korona.”

Nikataka kuongea lakini mwanaume yule akanifunga mdomo.

“Mmekuwa mstari wa mbele kupinga zoezi la chanjo ya Korona ambayo inatolewa na serikali. Sasa ni wakati wako kutueleza sababu za kupinga zoezi hili lisifanyike ndani ya vyombo vya usalama na hata kwa raia wa kawaida. Unaweza kutueleza sasa?”

Nilicheka baada ya maelezo hayo. Ni kweli nilishakataa jamii ya watu wa Tanzania kupatiwa chanjo ambayo madhara yake siku za usoni yanaweza kuwa makubwa.

Hatimaye nilipata ujasiri, nikasema, "Sikiliza wewe kibaraka. Mimi sijampinga mtu yeyote, ila nataka kuelimishwa zaidi. Ninachotaka kufahamu huenda ndicho kile kile ambacho raia wa kawaida wanapaswa kufahamu. Kuna tetesi na fununu nyingi kuwa chanjo hii inalenga kudhoofisha jamii ya watu weusi, na tuzidi kuongezewa mizigo ya kunyonywa kupitia afya, na si jambo la kuona athari leo—zitakuja kuonekana athari hapo baadae. Kwa hivyo napaswa kujibiwa kuwa, kwanini kumekuwa na uharaka wa kuwachanja watu kiasi hiki, tena muda wa kufumba na kufumbua? Na kama ni hiari, kwanini kuna masharti kuwa wasiokuwa na chanjo hawatapatiwa baadhi ya huduma katika

ofisi za umma na taasisi zake? Tena serikali imeenda mbali kwa kuwanyima huduma za msingi watu waliohiari kutochomwa chanjo. Kwanini tiketi za mabasi zinagawiwa kwa wenye chanjo katika baadhi ya miji? Kwanini wanafunzi wanakataliwa katika shule za umma wasipokuwa na kadi ya chanjo? Kwanini hata kitambulisho cha taifa letu sasa lazima kigawiwe kwa wenye chanjo? Na je, inawezekanaje mataifa ya nje yatupatie chanjo bure na pesa juu kama hawana manufaa ya muda mrefu na zoezi hili?" pia, hujiulizi kwamba jamii yetu inao watu wasiopungua milioni tisini, sasa kwanini wameleta dozi elfu moja tu kati ya watu wote hawa? Napata mashaka kuwa dozi hizo elfu moja ni mtaji wa kusambaza zaidi, yaani wakichanjwa hao ndio watakuwa waenezaji wa vimelea kwa jamii yetu hadi tuenee wote."

Yule bwana akababakia kimya.

“Nijibu? Kuna faida gani ya kuchanjwa kama bado naweza kupata maambukizi mapya na nitaendelea kuvaa barakoa na kutumia kemikali kutakasa mikono yangu kama tahadhari?”

“Sikiliza mpumbavu wewe. Hivi unajua kuwa sayansi haidanganyi? Chanjo si jambo geni ambalo sasa unapaswa kulihoji? Kuna chanjo za surua na polio zishatumika sana hapa nchini, iweje unaona hii haifai sasa?”

“Sijaona dhamira ya dhati ya jambo hili katika nafsi yangu. Na kama kuna dhamira ya dhati, bado natilia mashaka kuwa chanjo hii inafanyiwa majaribio kwa jamii yetu. Je ikiwa na madhara makubwa siku za usoni? Hayo yote sawa, lakini kwa akili zangu nadhani inafanyika hivi kwa sababu ya ubinafsi wa viongozi wetu. Wanataka kupata misaada kwakuweka rehani maisha yetu. Kwanini ubinafsi uleule walionao wawakilishi wetu hasa wabunge, wa kuwa wawakilishi wanaotumbua nchi usiendelee

pia katika chanjo. Ilifaa kabisa wakatuwakilisha hata katika jambo hili. Wakadungwa chanjo kisha tukaona mienendo ya afya zao kwa kipindi cha matazamio ndipo kama inafaa basi sisi wanaotuwakilisha tukajua kama inafaa au la!"

Mwanaume yule akaguna.

"Maneno kama hayo ndiyo yanayowachukiza sana waliotutuma. Hivyo kwa hapa ulipo tutakudunga chanjo kwa lazima, wewe na mtoto wako, pia huyo mkuu wako wa kitengo. Nadhani tukifanya hivyo mtatulia na kufunga bakuli na kuacha kuzua mijadala ya kutukwamisha katika zoezi hili. Kumbuka kuwa chanjo hii italeta manufaa makubwa kwa nchi. Kuipinga ni sawa na kuhujumu uchumi. Tutakosa mafungu ya fedha kutoka kwa wafadhili na uchumi utaharibika vibaya katika nchi hii."

"Chanjo ni hiari! Ikiwa lazima sipo tayari, labda mniue mkitaka, ila ukweli nitausema."

Maneno yangu yakamkasirisha sana mwanaume yule. Akachukua jukumu la kuniadhibu kwa ngumi na mateke mazitomazito.

Nilipokuwa nimelegea ndipo nikajumuishwa katika chumba kimoja na mtoto wangu Allen, pamoja na mkuu wangu wa kitengo, Kachero Frank.

Tulikuwa tumefungiwa ndani ya chumba kimoja kikubwa, ambacho kwa kukitazama kilikuwa kama bohari la kuhifadhia pamba, ila sikuwa na uhakika mahali tulikuwa kijiografia: sikujua kama ni wapi.

# 3

Bado msimamo wangu ulikuwa umebebwa na hiari ya kuamua. Hata siku moja hiari haiwezi kuwa lazima. Sasa nilipobaini kuwa waliotushika ni watu waliotumwa na serikali ya nchi yetu, sasa nilielewa kilichokuwa kinaendelea. Ni kweli kwa muda mrefu kidogo nimekuwa nikipinga harakati za wazungu, zile zilizotaka sisi raia wa Tuvumiliane tukubali kupatiwa chanjo za majaribio kwa ajili ya kuzuia kusambaa kwa kirusi kilichotajwa kuwa cha Korona.

Si peke yangu nilipinga hoja hiyo, bali hata mkuu wangu wa kitengo, Kachero

Frank naye alipinga vikali hoja hiyo kwa maana ni wajibu wetu kama kikosi maalumu cha wapelelezi tunaofanya kazi nje ya mfumo wa serikali kusimama kidete na kuingilia mahali ambapo tunaona maslahi ya raia wa Tuvumiliane yanaingiliwa. Sisi ni jicho la raia hata baadhi ya viongozi wanaoweza kuonewa. Kilicholeta utata katika fikra zetu ni ukweli kuwa, chanjo iliyokuwa ikisambazwa ilikuwa inatiliwa mashaka kila kona ya ulimwengu. Si hivyo tu, kama chanjo ingefaa ikawa moja iliyoidhinishwa, kilichotia mashaka zaidi ni utitiri wa makampuni kutoka Ulaya na Amerika yakiwa na dozi za chanjo aina mbalimbali. Akilini ikajengeka dhana kuwa makampuni hayo yanashindana kutafuta uhalali wa kuliteka soko la tiba katika bara zima la Afrika.

Shaka nyingine ni kwamba, hata sasa hao walioianzisha chanjo huko ng'ambo

kuna baadhi yao wanaipinga vikali na kutoa sababu za kupinga kwao kuwa haina manufaa yoyote kwani ni mrija mpya wa kinyonyaji unaonuia kutengeneza mazingira ya hofu kwa nchi nyingi ikiwemo Tuvumiliane ili kuweza kunyonywa raslimali zake kwa propaganda za chanjo. Ila ukweli utabakia hai kuwa; sababu ya hofu, ujinga na ulimbukeni pia ubinafsi wa viongozi wetu ndipo tutaweza kuangamia kama ilivyokuwa kwa ugonjwa wa UKIMWI. Hata siku moja, haijawahi kutokea kuwa chanjo inazua ugonjwa wowote. Kwa binafsi yangu naelewa kuwa chanjo dhidi ya ugonjwa fulani hutolewa ikiwa na vimelea vya ugonjwa huo ambapo ukichanjwa kinga ya kimelea hicho kwanza utaambukizwa kimelea cha aina hiyo ati kiwe mlinzi wa kuwazuia vimelea wa aina hiyo kukushambulia. Uonevu mkubwa. Hakika sikuwa tayari kuvuruga mfumo wangu wa mwili kwa kemikali zilizoandaliwa na makampuni yanayolenga

kuwafanya mataifa huru watumwa wa kutumia kuchota raslimali zao kwa kubadilishana na chanjo. Makampuni ya chanjo ni wafanyabiashara wanaoshirikiana na serikali za mataifa mbalimbali ili kujichotea utajiri wa mataifa ambayo wao huyaita dhaifu.

Nilienda mbali kuwaza kama kweli inawezekana mimi Raymond Masele, alimaarufu Chato kama nitaweza kupoteza uhai wangu kizembe namna ile kwa tatizo la mafua tu, ama changamoto ya kupumua. Kamwe jambo hilo siliafiki hata kidogo. Ninapojaribu kurejea historia ya maisha yangu nikiwa hapo kizuizini naona mnyororo wa maisha yetu ya utoto hadi utu uzima. Tangu kuzaliwa kwangu, maisha yetu ni ya vumbini; topeni; ya jua kali; kula jalalani na makombo ya kugombania na wanyama; na magonjwa ambayo kwetu si jambo la kustajabisha. Nikaamini hoja ya mtafiti mmoja aitwaye Andreas Moritz

kuwa, virusi ni sehemu ya maisha yetu, tena havina madhara kwa afya kama kinga asili ya mwili haijavurugwa.

Huwa tunaugua mafua na tunapona bila hata kipande cha dawa. Maisha ya kulala vumbini na tunapumua bila tatizo usiku na mchana tulishazoea, iweje leo kuwe na changamoto ati kwa kisingizio kuwa kuna kirusi ambacho kitaathiri afya zetu. Hapohapo nikajiuliza, kama hakuna chanjo dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI hadi leo, ugonjwa uliotokana na hila za wazungu kuidhoofisha Afrika, iweje hii ya Korona ije haraka namna hii na kuzisisitiza jamii za watu kuchanjwa?

Ubatili.

Nikabaini njama chafu tena ya wazi ndani yake. Kwa sababu ni haki pia uhuru wangu kuzungumza, nikaona yaweza kuwa wazungu wanaandaa mazingira ya kuvinufaisha vizazi vyao kwa miaka ya mbeleni na si kwa sasa. Wao huwa na tabia

ya kuandaa hatima ya siku za usoni kwa vizazi vyao kwa muda mrefu. Sisi huandaa mazingira yetu kwa wakati huo—yaani huchumia tumbo kwa ubinafsi na hakuna afanyaye jambo kwa manufaa ya kizazi chake kwa miaka kadhaa ijayo. Tumelala. Tunaongozwa na tamaa ya muda mfupi, kwa ubinafsi wa kizazi tulichopo. Sasa huenda chanjo wanazotudunga leo zitajibu kwa kutokea madhara, hasa magonjwa tusiyoyajua huko mbeleni huku wao wakiwa tayari wanajua watatuuzia dawa kwa kubadilishana na raslimali zetu adimu. Ama wanaandaa mateka wa kitekinolojia ambao watakuwa wa manufaa siku za usoni.

Nilipokuwa nimefungwa sasa damu nikahisi kuchemka zaidi.

Hasira.

Kifua kikatuna na mishipa ya kichwa ikasimama wima. Nilipowaza kuwa nadungwa sindano ya chanjo, sindano ambayo inao vimelea wa Korona mwili

wangu utakuwa dhaifu, na kinga yangu ya mwili wa kiafrika itashuka na ndipo naweza kupoteza maisha muda wowote…nikajikuta najawa nguvu.

Nikataka kujitetea.

Wakati huo yule mwanaume aliingia katika bohari akiwa kaongozana na Nora—mwanamke mrembo wa umbile ila mbaya wa sura. Nilipoona kavalia glovu nyeusi na kushika chupa ndogo ya rangi ya ugoro pamoja na bomba la sindano nikajua sasa ni wakati wa kujitetea. Mtoto wangu ambaye ni Allen nilipomtazama ni wazi alinitaka nifanye jambo kwa jinsi alinitazama. Nikamtazama Kachero Frank ambaye ni wazi hakuwa na nafasi ya kujitetea kwa jinsi alikuwa kalegezwa kwa kipigo. Hapo ndipo nikaona Nora anavuta dawa iliyokuwa kwenye kichupa na kujaza bomba la sindano aliyokuwanayo. Akanitazama kisha kumtazama Allen huku akipiga hatua kumfuata. Allen alipiga kelele ambazo

zilifanya apatiwe kipigo kikali cha kushtukiza na mwanaume yule ambaye nilitamani kuinywa damu yake. Sikuwa tayari kuona mwanangu akichomwa sindano ile nisiyokuwa na uhiari nayo.

Ingali mishipa yangu ya mwili imevimba, nikaona Nora anamwelekea Kachero Frank. Muda huo akamsukuma na kumfunua sehemu ya bega lake ili amdunge ile sindano. Nilipokagua kwa haraka, mahali nilikuwa nimeketi, kwa chini palikuwa na nondo moja nene, ambayo ilitumika kumtesa Kachero Frank. Nikajiwa ujasiri wa kuitumia miguu yangu iliyokuwa tayari huru kwa kuibana nondo ile na kuipishanisha, kisha nikaituma kuruka hadi mahali Nora alisimama tayari kabisa kumdunga sindano Frank.

Kilichotokea ni cha kustaajabisha hata mimi sikuwa na uhakika kama ningefanikiwa. Nilikuwa nabahatisha tu. Kwa ghafla mno Nora nilimshuhudia akiwa

sakafuni akilalama kwa sauti kali. Nondo ile ilipiga ile sindano aliyokuwa kaishika. Sindano ikamchoma kisha nondo ikajibamiza kwenye sakafu na muda uleule iliruka na kumchoma sehemu ya jicho lake la kulia.

Kelele zile zilimkaribisha mwanaume yule ambaye alikuwa na mwili uliojengeka. Nikajua ujio wake utakuwa wa mtu aliyekanganyikiwa. Nilijivuta haraka na kubana pembeni ya mlango nikiwa natumaini miguu yangu kunifanyia muujiza. Niliposikia vishindo akija nikajiweka sawa kumshambulia. Hapo ndipo nilipofanikiwa kumnasa na kumwangusha ambapo nilimpiga kabali kwa kumzungushia miguu yangu kama chatu. Nilinuia kumuua kabisa ambapo nilipoona kalegea nikaling'ata koromeo lake kwa meno yangu na kutema damu kando. Pande yule wa mtu akabakia kutapatapa sakafuni nikishuhudia namna alikata roho kizembe.

Nilipoangaza macho kumtazama Allen, sura yake ilinionyesha hofu aliyokuwa nayo kutokana na kitendo kile alichokiona pale ndani. Nilichokifanya hakikustahili kuonwa naye kwani lazima kisaikolojia kilijaa ukatili kwa mtoto kama yeye. Nilitingisha kichwa kisha nikajivuta na kusogea mahali penye nguzo nikafanya harakati za kuikata kamba niliyokuwa nimefungwa. Ilinichukua muda mfupi sana kujiweka huru. Hapohapo nikamfungua Allen mikono yake na ndipo nikaelekea kwa Frank ambaye sasa alikuwa karejewa na fahamu japo kwa mbali.

Wakati natafakari mahali pa kupita ili kuiepa kadhia ile kwa kutoroka, kwa ghafla mno nilisikia vurumai kwa nje ya bohari ile. Ni dhahiri kulikuwa na watu waliokuwa wanakuja. Yalikuwa mawili: Ni askari ama raia walipata taarifa zile na walipaswa kufanya lolote.

Nilipotaka kujiweka sawa tayari kwa kukabiliana na yeyote, lango la bohari ile

nikaliona limefunguka. Nikaona askari wawili wenye silaha wamesimama mlangoni na wakatoa onyo kuwa asitokee mtu wa kufanya hila yoyote dhidi ya wanausalama wa mahali pale. Nikanyosha mikono juu na kushika kisogoni wakati watu wale waliovalia magwanda ya jeshi la Tuvumiliane wakiingia kwa umakini mkubwa. Sikuwa na silaha ya aina yoyote kwani nilitaifishwa mapema na akina Nora.

# 4

Zilikuwa zimepita siku tatu tangia nifanye mauaji ya askari wawili waliokuwa wakihusiana na serikali moja kwa moja. Nora na Panda ndio niliwaua katika bohari la kuhifadhi pamba la ukanda wa Nyanza, kusini mashariki mwa Tuvumiliane. Siku ile ilikuwa ngumu na sikuwa nimefanikiwa kupata usingizi kwa takribani siku tatu mfululizo baada ya kuwa tumechukuliwa kutoka pale na kikosi chetu cha Silent Detectives (SD) kikiongozwa na Kanan. Askari waliotuchukua mahali pale walikuwa ni miongoni mwa watumishi wenzetu, ambao tulifanya kazi bega kwa

bega, na huenda walinusa harufu ya kutekwa kwetu na wakafuatilia mienendo yetu hadi kufika mahali tulikuwa tumehifadhiwa kwa wakati ule.

Sasa kukawa na mazingira hatarishi kati yetu na kundi la mashushushu wa serikali ambao walipewa agizo kali la kutaka kutuangamiza. Kikosi chetu kilikuwa na askari wanane tu nchi nzima, ambao kwa dhati tulikuwa tukifanya kazi kwa weledi mno. Mara tu baada ya kuonesha uasi wetu dhidi ya maamuzi ya serikali, kwa kupinga uamuzi wa kuwapatia chanjo wananchi wa Tuvumiliane, sasa kulitolewa tangazo la wazi kuwa kuna msako wa kuwanasa wasaliti. Idara ya usalama ya serikali ilitoa notisi ya sisi kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria ama kuuawa kama tutakaidi agizo la mkuu wa kitengo cha upelelezi. Ulikuwa wakati wa kuweka kando kila kitu na kuanza kupigania uhai wetu.

Jambo nililoliwaza kwa haraka lilikuwa ni kuisafirisha familia yangu na kuipeleka nchi jirani ambako kulikuwa na rafiki yangu wa siku nyingi. Hivyo usiku wa siku ya tatu baada ya tangazo hilo la kuwa tunasakwa, nilimchukua Allen pamoja na mamaye, nikawapeleka katika bandari ya nchi yetu ambako hupakuliwa makontena na kubebwa hadi nchi za jirani. Nilichokifanya ni kuongea na dereva wa lori nikampatia kiasi cha pesa ili awasafirishe kuelekea nilikokuwa nimepanga na wakapokelewe. Nilipofanikisha hilo nikampigia simu rafiki yangu Jamshid na kumjuza kuwa familia yangu aipokee mpakani na ajue namna ya kuisitiri kwani nilikuwa naingia katika mapambano yasiyo na huruma. Jamshid alikubaliana nami, nikampa namba ya dereva wa lori na namba za simu za mke wangu na kuwatakia safari njema.

Palipopambazuka tulikuwa katika moja ya mji wa kale ulioko katika pwani ya nchi

ya Tuvumiliane. Huko tulikuwa watano tukipanga namna ya kukabiliana dhidi ya agizo la kutaka tukamatwe ama tuuawe kwa sababu ya kukaidi miito ya serikali iliyolenga kuangamiza raia wake kwa chanjo bila kujua athari zake.

"Nimewaita hapa ili tule kiapo kwa ajili ya maisha yetu na hatima ya tunaowatetea. Si kila wakati serikali ikawa sahihi. Kuna wakati inakosea kwa sababu ya udhaifu wa viongozi ilionao, au la inakosea kwa makusudi kwa sababu ya kujitafutia misaada isiyo na manufaa kwa taifa. Yapo mambo inakosea, ikikwama inawatoa kafara wananchi wake. Wanasiasa si watu wazuri kwa maana wanaweza kuamua jambo lifanyike kwa maslahi yao ila si kwa maslahi mapana ya raia wasio na mamlaka. Kikosi chetu ni kidogo, lakini kinaweza kutuma ujumbe kwa kishindo hata jeshi zima likaingia vitani na kuangamia," alisema Kachero Frank.

“Ndiyo mkuu!” tuliitikia sote.

“Najua tunapambana na dola ambayo inalo jeshi kubwa. Njia tutakayoitumia ni kunyakua na kuua wanaoheshimika, hasa wanaoshikia bendera jambo hili la kuwafanya raia wachanjwe kwa vimelea visivyo na mantiki kwa afya. Propaganda wanayoieneza kuwa wamechanjwa ni hatari—ni uongo tu. Sasa tutaanza na watendaji wakuu, wote waliojitangaza kuwa wamedungwa chanjo hii. Kisaikolojia jamii yote ina hofu. Sasa yafaa wanasiasa wote waliojitangaza kuwa wamedungwa sindano ya chanjo wakati siyo, ttutumie propaganda ileile wanayoitumia, tuwashughulikie mmoja baada ya mwingine….na lazima vifo vyao viwe vya kufanana ili iaminike kuwa chanjo waliyopokea haifai. Bila hivyo watatushinda nguvu. Wakipoteza maisha kwa wingi na kwa mfululizo jamii ya Tuvumiliane itaamini na itaasi kwa

kuipuuza serikali iliyopo,"aliendelea kusema Kachero Frank.

Niliamua kuuliza… "Mkuu, njia ipi ya kufanana itawaua watu hawa na isitambulike na serikali kama kuna hujuma nyuma yake?"

Tulipanga mipango kabambe kwa kubadili tabia zetu. Kilichokuwa kimeafikiwa ni kutafuta sumu ambayo wangevutishwa kisha wangepoteza maisha muda mfupi baada ya kushindwa kupumua."

Hapo ikatolewa orodha ya kila mlengwa wa kutekwa na kuuawa, hasa wanasiasa waliokuwa mstari wa mbele kuwaaminisha raia kuwa chanjo ya Korona ilikuwa salama kumbe hawakudungwa sindano yoyote ya chanjo hiyo. Ni kundi la viongozi waliopokea pesa kutoka katika makampuni ya kuzalisha chanjo ili wawe wakala wazuri wa kuhakikisha wananchi wanakubali kupokea chanjo ili makampuni yajivunie pesa ya kutosha na kuwaacha wananchi

wenye hali duni hawajiwezi kiafya na kiuchumi.

Siku ya pili kwa haraka mno tulibadili mienendo ya maisha. Tulikuwa tukibadili mavazi na kuvaa mabaibui na kujitanda kama wanawake wa kiislamu. Kuna wakati tuliishi katika makasino na kuna wakati tuliishi makanisani na misikitini kwa mitindo mbalimbali. Kikosi chetu kikaanza utekelezaji wa kuwaangamiza waliokuwa katika orodha yetu. Tukaanza na kiongozi wa chama kilichokuwa cha upinzani, ambaye hapo awali alishikia bango kuletwa kwa chanjo ile. Tulipomnasa akiwa katika starehe za usiku tulimvutisha sumu ile na siku ya pili alikutwa kaanguka katika maliwato ya klabu moja ya usiku. Na uchunguzi ulipofanyika ikawa wazi kuwa alikufa kwa sababu ya shinikizo la damu baada ya kushindwa kupumua.

Vilevile tukaendelea kuwawinda watendaji wakuu wa serikali ambao

walijitangaza kupata chanjo ile huku tukijua kabisa kuwa hawakuchomwa chanjo ile, wakiwahadaa raia. Tukafanikiwa kuwaangamiza mawaziri watatu mfululizo na wakuu wa wilaya na mikoa wasio na idadi kwa wingi. Hapo ndipo taharuki ikaongezeka kwa jamii. Kila raia akahoji juu ya vifo hivyo vya ghafla tena kwa kufuatana.

Raia wengi wakajenga dhana hasi dhidi ya chanjo ile na kuyalaumu mashirika ya kimataifa yaliyokuwa yanatoa chanjo kuwa yamelenga kukiangamiza kizazi cha wanyonge kote duniani. Waliokuwa wamejitokeza kupatiwa chanjo ile nao wakazidiwa na mashaka kuwa wangepoteza maisha muda wowote. Wakawa katika mhaho usio na kipimo wakisaka kujinusuru kwa kutafuta njia mbadala za kuweza kuondosha kemikali ile miilini mwao kwa haraka.

Muda wa yote hayo hatukuwa tumekamatwa hata mmoja wetu, ila siku

iliyokuwa imefuata ndipo nilipata habari mbaya za kuuawa kwa askari wenzangu wawili wakiwa katika misheni huko katika mikoa ya mabondeni. Kachero Frank akanidokeza kuwa tayari kulikuwa na nguvu ya ziada ilitumika kwa kukodi askari kutoka nchi jirani ili wasaidie kupambana na kundi letu lililoasi. Pia kukaja fununu kuwa, serikali ilikuwa na mpango wa kuomba wapelelezi mahiri kutoka mataifa ya ulaya na Amerika ili wafanye uchunguzi wa kuweza kutukamata kwa muda mfupi.

"Inafaa kubadili namna ya kuishi. Sasa inabidi tubadili mbinu. Yafaa tutafute makazi nchi jirani, tuwe tunafanya kazi zetu kwa kushtukiza kisha kwenda mafichoni.." alisema Kachero Frank.

Wakati anamaliza kusema hayo kwa simu, nilipokea simu nyingine. Sasa ulikuwa muda kidogo umepita tangu mke wangu na mwanangu Allen waende nchi jirani kwa lori. Nilipata habari walipokelewa

kwa mafanikio na walikuwa wakiishi bila wasiwasi. Lakini baada ya simu ya Frank kukatika, nikapata habari mbaya kutoka kwa rafiki yangu, bwana Jamshid.

"Bwana Chato, nasikitika kukujuza kuwa Allen na mama yake wametekwa na watu wasiojulikana."

"Unasemaje, Jamshid?" niliuliza kwa hofu.

"Wametekwa!"

Nikahisi mapigo ya moyo kwenda mbio. Nilikata simu ili nitafakari namna ya kufanya. *Wametekwa na nani? Ki-vipi wametekwa wakati Jamshid ndiye alibeba dhamana yao huko ugenini?*

# 5

Kusikia mke wangu na mtoto wametekwa tena katika nchi ya kigeni kulininyima furaha kabisa. Sasa nikajawa mauzauza. Nikaweweseka huku na kule. Amani yote ilitoweka moyoni. Nikawa najua fika kuwa kati ya waliofanikisha kutekwa kwa familia yangu miongoni mwao atakuwemo Jamshid. Amenisaliti. *Imekuwaje askari wa serikali wakapata fununu na taarifa hizo kuwa wapo nchi jirani na kufanikiwa kuwateka?* Nilijiuliza.

Ningali katika kuwaza, nikajikuta naelemewa na mawazo. Nikajilazimisha kwenda katika klabu moja ya usiku iliyo

karibu na kwangu. Nilichokifanya siku ile ni kujimiminia kilevi kiasi ambacho sikuwa na wasiwasi hata kama nitakamatwa na kuwekwa kizuizini. Kama cha thamani kwangu ni mke na mtoto wangu, mimi nilikuwa wa thamani gani tena hata niogope na kuyajali maisha yangu peke yake? Niliokuwa nawatetea katika unyonge ni watu wa Tuvumiliane wote, hasa familia yangu ikiwemo. Sasa kama wametekwa ni lipi litanifanya niwe na hofu kwa kuyatetea maisha yangu? Niliwaza sana namna ya kufanya lakini nikakosa jibu la haraka.

Nchi waliyokuwa familia yangu ni ngumu kuingia kienyeji, hivyo ilikuwa lazima tu nifanye jambo la ziada kuweza kuingia huko. Kwanza ilinipasa kuwa na hati ya kusafiria, pia niwe na hati ya kunitambulisha kuwa nimedungwa chanjo dhidi ya Korona. ukweli sikuwa na uhiari wa kutii sharti la chanjo kwanza ndipo nipatiwe viza ya kusafiria. Japo nilikuwa na

pasi ya kusafiria tayaritayari, sikutaka kutii sharti hilo gumu. Isitoshe wakati huo nilikuwa miongoni mwa wanaotafutwa na serikali, sasa ningewezaje kuingia katika ofisi za umma na kupata viza kama si kujisalimisha mwenyewe.

Jambo jingine ni kwamba, serikali ilikuwa imeshachukua hatua za kututia kizuizini ikijua kwamba tupo bado ndani ya nchi, hivyo ilizifuta hati zetu za kusafiria ili tusikimbilie mahali popote. Kwa maana hiyo, hata hati yangu ya kusafiria ilikuwa batili tayari.

Nilipokuwa nimeketi nilitafakari jambo la kufanya. Nilipokumbuka kuwa lugha waitumiayo watu wa nchi niliyowaza kwenda na ambako niliwapeleka watu wangu, nami naijua vema ndipo nikapata ahueni fikrani. Ikanilazimu sasa kusafiri usiku uliokuwa unafuata kwenda moja kwa moja hadi katika mpaka wa nchi yetu ya Tuvumiliane na nchi jirani ya Kisirani. Hapo

nikapiga kambi katika ofisi za uhamiaji nikiwa najaribu kunusanusa. Nia yangu ni kuwachunguza watu waliokuwa wakiharakati kuingia nchini mwetu kutokea nchi jirani. Nia yangu pia ilikuwa ni kumnasa raia yeyote wa kutokea Kisirani na kumficha mahali ili hati yake aliyoidhinishiwa pamoja na cheti cha kuwa kapokea chanjo ya Korona viniingize ndani ya nchi hiyo ili niweze kufanya upekuzi wa kuitafuta familia yangu. Sikuwa namwamini tena Jamshid, zaidi nilitaka yeye awe wa kwanza kunisaidia kuwajua walioteka familia yangu.

Pale mpakani hali ilikuwa ngumu sana kupapita. Masharti ya kuvuka na kwenda upande wa pili yalikuwa magumu sana kwa sababu ya vielelezo vilivyohitajika. Isitoshe, kutambuana kwa uwazi ilikuwa vigumu mno hasa kutokana na kila mmoja kavaa barakoa kwa kufunika pua na mdomo wake

hivyo kupunguza uwezekano wa kutambuana kwa urahisi.

Japo palikuwa na vurugu za hapa na pale, nilibahatika kumpata mwanaume mmoja aliyeingia upande wa Tuvumiliane akiwa kama mfanyabiashara. Sura yake haikuwa mbali kabisa na yangu. Alikuwa mrefu kama mimi. Kichwa chake kilikuwa cha duara kama mimi. Macho yake yalikuwa kama yangu kwa udogo. Rangi ya ngozi yake ilikuwa maji ya kunde kama mimi. Umbile na mjengo wa mwili wake ulikuwa wa misuri ya wastani kama mimi. Huyo nikaona ni sahihi kumhujumu ili hati yake isaidie kuniingiza nchini Kisirani kwenda kufanya msako wa hayawani walioteka familia yangu.

Basi, niliifuatilia mienendo ya mtu yule hadi akagongewa viza na kuhakikiwa kwa cheti chake cha chanjo. Alipanda basi nami nikapanda hilohilo. Kwa uzuri zaidi nikaketi naye katika viti pacha. Yeye aliketi dirishani

nami kuketi mwanzo kabisa wa korido iliyotengwa na viti vya basi lile kutoka pale mpakani kuelekea kwenye jiji la Joto alikokuwa akielekea.

Safari ile ilikuwa ya saa zaidi ya nane hadi kufika mji mkuu wa Tuvumiliane. Kilichotokea ni kusoma mienendo yake yote. Nikawaza kuziiba nyaraka zake lakini nikasita maana ingekuwa hatari zaidi kwani angeweza kutoa taarifa popote na hata nikitaka kuzitumia ningetiwa mbaroni. Nilipotaka kumuua ama kumlewesha napo nikashindwa, ikabaki dhana moja akilini mwangu kuwa sasa nitafute namna ya kusafiri naye hadi mwisho wa safari. Huko nikafanye namna ya kumteka na kumhifadhi huku nachukua nyaraka zake ili zinisaidie.

Safari yetu sasa ilikuwa ndefu mno. Tulifika katika jiji kuu la Tuvumiliane saa 5 usiku. Kwakuwa alikuwa mgeni akalazimika kuniuliza mahali tulivu

ambapo angeweza kupumzika. Nikamwelekeza mahali panapofaa na nikajitolea kumpeleka katika hoteli moja iliyo kando ya vurugu za jiji.

Huko nami nilikodi chumba cha pili kutoka katika chumba chake. Kwa namna alinizoea tulipiga gumzo la hapa na pale kabla ya kulala. Nikamweleza kuwa inanipasa kulala hapo kwani ilikuwa vigumu kwa usiku ule kwenda nje ya mji ambako ndiko nyumbani kwangu kwa sababu usiku huo hapakuwa na usalama wa kutosha hadi pawe na pambazuko. Bwana yule akaniunga mkono juu ya uamuzi wangu.

Niliingia chumbani mwangu na kujilaza kitandani huku natafakari namna ya kufanya. Nikapanga kuwa usiku uleule lazima nikamilishe misheni. Mbinu niliyoipanga ni kumwita askari mwenzangu aje na sare za uhamiaji mahali pale. Nilitaka amchukue bwana yule kama mhalifu ndipo

tupate mwanya wa kuchukua vielelezo vyake na kuvifanyia kazi haraka.

Nilipompigia simu bwana Kanan, alikuja kweli kwa wakati kwani alikuwa anajua kila hatua ya safari yangu na ujio wa yule mgeni. Akaomba kukagua vyumba vya wageni waliokuwemo hotelini mule likiwa lengo ni kumnasa bwana yule kutoka nchi ya Kisirani. Alipofika katika safu ya ghorofa tuliyokuwa na vyumba ndipo akagonga kwa mgeni niliyekuwa nimemweleza. Akamtaka kutoa vielelezo ambavyo alivikagua. Kanan kwa makusudi tu akasisitiza kuwa mgeni yule alikuwa na vielelezo bandia. Nilizisikia vurumai wakibishana nikiwa chumbani mwangu wakati mgeni yule akisisitiza kuwa vielelezo vyote vilikuwa sahihi. Kwa ushahidi zaidi mtu yule akaona ni msaada kwake hivyo akataka niamshwe ili nisaidie kutoa maelezo kwakuwa tulikuwa sote tangia tunatoka mpakani. Kanan akanigongea mlango ambao alijua kabisa nilikuwamo. Tukawa kama hatujuani na Kanan

ila yule mgeni. Yule mgeni akatoa maelezo yake nami nikawa kama namtetea ndipo Kanan akasema, “Tutamchukua hadi sehemu tunapowashikilia watu kama yeye. Hati yake ya kusafiria na vielelezo vyote tunavizuia hadi hapo utata utakuwa umeondoka. Tunafanya hivyo kwa nia njema tu—ya kulinda usalama wa ndani ya nchi yetu. Ni kipindi sasa kuna matukio ya kustaajabisha hapa kwetu, hivyo lazima tuchukue hatua kila wakati.”

Kwa hila tu, mtu yule akachukuliwa na kwenda kufichwa katika maskani ya ufukwe ambako tulikuwa na handaki kwa ajili ya harakati zetu.

Usiku uleule niliondoka na boti ya wavuvi na kuambaa ndani ya Bahari kuelekea pwani ya nchi jirani ya Kisirani nikiwa na vielelezo vile vya mateka wetu. Nia yangu ilikuwa moja tu, kumtafuta mke wangu na mtoto, kwa udi na uvumba.

# 6

Palipopambazuka nilikuwa katika ufukwe wa nchi ya Kisirani nikiendelea kupanga mikakati yangu. Sikuwa na wasiwasi hata kwani tayari nilikuwa na hati ya kusafiria iliyonitambulisha kuwa ni raia wa nchi ya Kisirani. Si hivyo tu, pia nilikuwa na kadi ya kunitambulisha kuwa nilikuwa nimechoma chanjo ya Korona. Jina langu sasa si Raymond Masele au Chato, bali nilikuwa Steven Nyantilu Ouko. Jina hili ndilo lilikuwa katika hati yangu ya kusafiria ambayo hata picha yake kwa muonekano ilikuwa imefifia na kufanya sura ile ionekane kama ni ya kwangu baada ya kuichezea kidogo.

Jua lilipopanda ngazi na kuanza kuumulika mji wa pwani nilielekea stesheni kwenda kupanda treni. Nilitaka kutoka

katika mji wa pwani na kuingia katikati ya mji mkuu wa nchi ya Kisirani ambako ndiko Allen na mama yake walikuwa wakiishi kabla ya kutekwa. Bado nilikuwa na kumbukumbu za kila mahali hasa mahali alipokuwa akiishi Jamshid na mahali alipokuwa akifanyia kazi. Makazi yake yalikuwa mtaa wa Magunia ambapo kuna makazi ya watu wa kipato cha kati kama Jamshid, na biashara zake alifanyia katikati ya mji, akiwa ni mmiliki wa klabu ya usiku kwa jina la El-Nino Night Club.

Nilipotazama saa yangu, likiwa treni linachanja mbuga, ilikuwa tayari saa saba, takribani tulikuwa tumekata saa tano tukiwa njiani. Nikajitahidi kuwaza nje ya safari ile lakini ikawa vigumu kuacha kujiwa na hisia kali za kuwakumbuka wapendwa wangu. Wakati ule sikutaka tena kupiga simu popote kwani namba niliziandika katika karatasi nikiogopa kufanya mawasiliano ya moja kwa moja.

Katika treni, tulipokaribia stesheni ya jiji la mji mkuu wa Kisirani nilikuwa tayari nimefanikiwa kumpora simu msichana mmoja aliyekuwa jirani yangu, ambaye alikuwa kalala usingizi wa fofofo na kuiacha simu yake ikizubaa kwenye kiti. Muda huo akiwa kalala bado nilielekea msalani katika treni lile ambako nilichana kapeti la ukutani na kuificha ile simu baada ya kuizima. Nilijua kitakachotokea si cha kawaida kama sitafanya ujanjaujanja kama ule.

Niliporudi kitini ndipo msichana yule akawa amezinduka nami nikiwa nimejidai kushikwa usingizi. Alipojipapasa akaiona simu yake kubwa, lakini simu ndogo hakuwa nayo. Akajikagua mara kadhaa kisha nikaona ameduwaa akitafakari. Hapo ndipo nikajua hakuwa na uhakika wa kile aliwaza. Nilijifanya nagutuka, kutoka usingizini. Nikamsemesha.

“Vipi, kuna nini mbona unawaza sana?”

“Nimepoteza simu yangu?”

“Simu? *Smart phone*…au?”

“Hapana…ni kiswaswadu tu cha tochi..lakini …basi tu..”

Nikasimama pale kitini na kuanza kuinama kukagua hapa na pale hadi uvunguni mwa kiti.

“Usihangaike kaka yangu…..nahisi nitakuwa nimeisahau kwenye basi wakati nakuja kupanda treni pale Pwani.”

Nikajidai nashtuka.

“Unaweza kuipigia ili tujue kama ipo *on*?”

Akakubaliana nami. Akabofya namba zake kisha kitufe cha kupiga. Namba ikawa haipatikani tena. Ujumbe uliokuja ulikuwa wazi kwamba namba aliyokuwa akiipigia ilikuwa haipatikani.

“Kaka acha tu. Ingekuwa hii kubwa ningepatwa wasiwasi, lakini hicho kitochi hakuna shida. Nitanunua kingine.”

“Hujui thamani ya simu kuwa ni namba za simu zilizomo…..hujutii kuzipoteza?”

“Hata sina wasiwasi. Majina yapo kwenye *google drive,* pia kwenye simu hii kubwa. Sijapoteza kitu cha maana. Aliyeokota naye riziki yake.”

Basi tukawa tunaingia stesheni huku nikiwa nawaza mara kadhaa jinsi ya kuingia mji ule wenye watu wengi na makundi-makundi ya askari yakiwa yamezagaa. Nikajiwekea barakoa yangu baada ya kuona ‘kashkash’ waliyokuwa wakipatiwa watu ambao walipuuza kuvaa barakoa eneo lile. Kwakuwa msichana yule alikuwa na mizigo ilinilazimu wakati wa kushuka nimsaidie. Tukapita lango la kutokea stesheni hadi mahali palikuwa na kituo cha magari ya abiria.

“Nashukuru kaka. Mimi naitwa Joyce Ouko!” akajitambulisha hata kabla sijamuuliza jina lake. Hali ile ikanifanya nipate mshituko kwa namna fulani hata ikanifanya kuweka tahadhari ya namna ya kujitambulisha kwake.

“Naitwa Steven Mwaniki!” nikajitambulisha.

“Ahaa! Nafurahi kukufahamu Steve…”

Nikamkazia jicho.

“Unaishi hapa jijini kati?” nikamuuliza.

“Naam. Nafanya kazi katika kituo cha mafuta, na sasa likizo yangu imeisha nimerejea.”

“Dah..ningekuwa na simu ungenipa namba yako, lakini si vibaya ukanielekeza kilipo kituo cha mafuta unapofanyia kazi ili siku moja nikutembelee.”

“Nafanyia kazi katika kituo cha Mwendokasi…barabara ya Lomolomo, kituo cha Total. Hapo ukifika uliza Joyce Ouko tu, utanipata.”

Nilitabasamu. Akatabasamu. Meno yake yalikuwa meupe yaliyopangana ndani ya kinywa utadhani askari wa kikosi cha wanamaji. Alikuwa mwanamke mrembo, pengine kumshinda hata mke wangu kwa

mwonekano wa nje. Alikuwa mweusi wa kung'ara, midomo yake ilikuwa ya kuvutia kama ua waridi changa. Macho yake yalikuwa malegevu utadhani alikuwa kaleweshwa kwa huba na kuchoka. Bado sauti yake ilinishitua nikatamani aseme nimsikie kwa jinsi ilimiminika kutoka kinywani mwake. Hakuwa na umbo kama kiroba, wala hakuwa na umbo kama sanamu la michelini, ila alikuwa na kiuno kilichomgawa katikati—kwa juu akajaza matiti makomavu yaliyosimama na kukigawa kifua chake. Makalio yake yalifanya vichuguu pacha nyuma yake na kufanya nitamani japo kumgusa.

Nilipovuta pumzi tu, ilitosha kushiba marashi aliyokuwa kayaogelea. Nguo alizokuwa kavaa zilitosha kunifanya mtumwa wa hiari kwa kumtazama. Si nguo za kuingilia ofisini, la hasha! Ni dhahiri zilikuwa nguo za mtu atokaye kula bata pwani. Alivaa blauzi nyekundu tepetepe

iliyoacha uwazi katika kifua chake na kufanya niushuhudie mjaziko wa matiti yake machanga. Kwa chini alivaa sketi *tetemente*—sketi iliyokuwa laini, yenye kutetema kila alipojihangaisha kwa kupiga hatua—ilikuwa fupi yenye mzunguko finyu.

Alipokuwa anapanda gari nilikuwa nimemkagua na kutathmini thamani yake yote kimaumbile. Ikatosha kuwa Joyce anafaa kuwa mwenyeji wangu ikibidi, na muda wowote ambao nitahitaji kuwa na mwanamke wa kuniliwaza basi nafasi hiyo inamfaa.

Nilimpiga jicho la kichokozi ambalo kwa mwanamke yeyote lazima atambue kuwa moyo wangu aliurarua na kuuacha hadi unalia kwa upweke. Hata hivyo, pamoja na kuwa nilikuwa katika mazingira magumu ya ugenini, nafsi yangu ilijikuta inataka kuzama katika hisia za mahaba kwa msichana yule.

Nikaikemea hisia ile iliyochipuka kwa kasi na kunifanya nikose utulivu. Joyce naye alijua kuwa mshale wa uzuri wake na mikogo aliyokuwa akiionesha kwa macho yake ulinipata pabaya. Alibaini kuwa nipo mahtuti na poyoyo kabisa mbele yake. Akiwa bado kanitazama vilevile kwa huba iliyojaa uchokozi, sasa akanikonyeza kwa mtindo ambao ilibaki kidogo nipoteze ujasiri wote niliokuwa nao.

Akatoa mkono wake kuuelekeza kwangu nikidhani sasa alifikia hatua mbaya ya kuniangamiza kwa huba. Nafsi yangu ikachekelea. Ikatatarika kama hindi lichomwapo kwenye moto mkali, ta-ta-ta-ta! Nilijua alikusudia niagane naye kwa kupenana mikono. Kiganja chake kiliponifikia nikahisi joto la ajabu katikati ya ngozi mororo iliyoteleza. Akaniminya kiganja changu chenye suguru za kiume huku kanikazia macho. Dole gumba lake likanitekenya juu ya kiganja na kuhisi

kupigwa na mkondo wa umeme ulioenda kuamsha maungo yangu sirini.

"Joyce!..." niliita tu hata bila sababu ya msingi, wala sikuwa nimemaanisha.

Akaitika ita yangu akisema, "Raymond—usijali tutaonana!"

Moyo wangu ulilipuka kwa hofu isiyo na mfano. Nikajikuta nabaki mdomo wazi. Nikaisikia sauti yake ikijirudia-rudia masikioni. Bado sikuwa naamini kama kweli aliniita kwa jina langu 'Raymond'. Nikabaki njiapanda kuwa huenda nimeingiwa uchizi na sasa nilikuwa naota kuitwa kwa jina hilo.

Joyce akapiga hatua kuondoka taratibu nikishuhudia mtikisiko wa vichuguu pacha nyuma yake. Alipotoweka ndipo nikalikumbuka tena jina la Ouko. Ni jina ambalo lilifanana sana na lile la kwenye hati yangu ya kusafiria. Nilisita kujitambulisha kwa Joyce kutokana na hofu, yaani huenda akawa nduguye, nikawa nimeingia matatani. Bado wasiwasi kuwa Joyce alinifahamu

ukabaki kuzunguka akilini hata nisijue ukweli wa nilichosikia. Kuniita jina langu halisi kulinipa wasiwasi sana.

Wakati nawaza uelekeo niliwaona polisi wakija upande niliokuwepo. Walikuwa kama wananifuata kwa namna walinikazia macho. Nikajizuia kuondoka na kubakia nimesimama mahali pale. Mapigo ya moyo wangu yakanienda mbio kiasi cha kusikika hata kwa masikio yangu mwenyewe. Nikawaza nipige hatua na niondoke mahali pale lakini nikajionya. Nafsini ukaja ujasiri wa ajabu kuwa nipo tayari kukabiliana nao kwani bastola yangu ilikuwa mahali pazuri, ambapo ni rahisi kuichomoa endapo ingenilazimu kuitumia.

# 7

Sikuwa na muda wa kupoteza baada ya polisi kunipita. Niliiingia mtaa uliokuwa mbele yangu, mtaa ambao ulikuwa na biashara za kila namna, hasa za vifaa vya kielektroni. Nikasimama katika kichochoro kimoja. Nikatazama nilikokuwa natoka. Hakukuwa na mtu wa kunishuku wala kumshuku. Nikaiwasha simu ambayo nilimpora Joyce kwenye treni. Baada ya kuiwasha ikawa ni wakati wa kujua majina yaliyomo. Nikashauku kujua kama jina lolote linalofanana na 'Ouko' lipo ndani ya simu ile. Nikajitahidi kuyakagua majina yote kwa kasi mno. Jicho langu likanasa

kwenye namba moja ambayo jina la mwisho ni Ouko. Jina hilo lilisomeka kaka Steve Ouko. Nikapigwa butwaa.

Ziliingia arafa kadhaa zikijuza kuwa kuna watu kadhaa walikuwa wamejaribu kumpigia Joyce. Kuna namba ya mwisho niliyoona ilijaribu kumtafuta na nilipotazama muda, ni ya wakati ule tunajaribu kuipigia. Hapohapo nikajua ndiyo namba ya Joyce. Nikaihifadhi katika simu ile.

****

Nilielekea katika mkahawa mmoja nikajipatia chakula baada ya kuhisi njaa kali ikinitafuna. Nilipokuwa natathmini mazingira ya jiji la nchi ya Kisirani, hakika niliona mambo ya kushangaza hasa kutokana na tahadhari za ugonjwa wa Korona zilivyokuwa zikisindikizwa na hasira za polisi. Mahali pale niliona watu wakiwa wamefunika midomo na pua kwa barakoa na haikuwa rahisi kuwatambua.

Nami ili kuficha sura yangu nisitambulike kwa urahisi nikaiweka barakoa kama wenyeji wangu baada tu ya kula chakula. Nikaanza kuutafuta mtaa ambao *El-Nino Night Club* ilikuwa ili nikaanze kumsaka Jamshid anisimulie kinaganaga juu ya kilichotokea.

*El-Nino Night Club* nilikuwa napafahamu. Sikupata shida kufika. Niliingia mahali pale ambapo nililazimika kujitambulisha kwa majina tofauti kwa kila aliyenichangamkia. Nikaagiza chupa ya mvinyo ili nipate kulipoza koo langu huku napakagua mahali pale. Nilichobaini ni hali ya utulivu na kuwashuhudia malaya kadhaa wakiwa wanaranda huku na kule. Wakati nataka kukata tamaa ya kumwona Jamshid ili nimwite mhudumu mmoja wa mahali pale na kumhoji, kama ngekewa tu, nikaona msichana mmoja mrembo kweli akitokea kwenye mlango wa pili uliokuwa ubavuni mwa klabu ile. Alikuwa mweupe, ni mrefu

wa wastani na sura yake imechangamka. Akatoka na mkoba kama kisanduku hivi ukiwa na nakshi ya dhahabu. Mkoba ule ni wa thamani kubwa kwa namna nafahamu bei yake dukani. Ulikuwa aina ya Flex MT. Mkononi alibeba pia koti jeusi la suti.

Baada ya sekunde chache kwa nyuma akatokea mwanaume mrefu na mwembamba. Alikuwa kavaa shati jeupe na kofia ya kahawia, ya duara. Macho yake hayakutazama pembeni, ila alizingatia hatua zake na kule aendako. Nilimtazama msichana aliyekuwa katangulia akielekea kwenye gari moja ndogo iliyokuwa mpya ikiwa imeegeshwa katika eneo ambalo ni la peke yake. Nilipotupa macho sawasawa, kwa pembeni, kwenye ukuta nikaona kibao kimeandikwa MKURUGENZI. Ilimaanisha kuwa egesho lile lilikuwa la mkurugenzi wa mahali pale, ambaye ni Jamshid Kilowoka, rafiki yangu wa miaka mingi nilipokuwa nchini Kisirani kwa masomo ya chuo kikuu.

Nilishangaa kumuona Jamshid akiwa kanawiri kiasi kile hata mavazi yake yashakuwa ya kitanashati mno. Fedha ilipiga kelele katika mavazi na mwonekano wake. Nikameza mate. Nikatazama namna aliagana na yule binti mwenye asili ya kiasia kwa kupeana mabusu mazito pamoja na kukumbatiana.

Jamshid aliondoka kwenye maegesho kwa mbwembwe. Gari yake maalumu aina ya Sport Lyndon ilitapika sauti kubwa. Ilikohoa kisha kutema cheche zikatapakaa kwa nyuma wakati inaondoka. Naujua ulevi wa Jamshid tangia barobaro—magari na yeye, yeye na magari. Kwake ngurumo za magari ni kama burudani. Akitoka asubuhi kwenda mazoezi ni ngurumo. Akienda kula mchana katika hoteli za kifahari ni ngurumo. Akienda jioni kwenye viota vyake vya burudani ni ngurumo. Na sasa alitokomea nikiwa naisikia injini pekee ikiwazomea walala hoi na kucheua cheche za ukabaila na

moshi wa fukuto la fedha alizokuwa akizichoma Jamshid katika njini ya gari lake. Pesa zilimtumikia hadi zikampa wazimu.

Niliachana na Jamshid na ngurumo zake. Sasa macho yangu yalihamia kwa msichana aliyeonekana kuwa ni kipusa cha kiasia—kifaa cha bosi. Nikajiambia pia kuwa namimi ni bosi kwa namna yake, na nastahili ukarimu wa binti yule kwa namna yoyote. Nikazifuata hatua za madaha za binti yule wakati anarudi ndani—yeye mbele na mimi nyuma. Wakati anausukuma mlango ili aingie niliudaka mkono wake wa kuume ambao ulipambwa na pete za bei ya kuruka. Akageuka kwa haraka na kunikazia macho akiwa kakunja ndita utadhani aliona kinyesi njiani. Watu walioniona nikimshika msichana yule wakaduwaa. Nikasikia wanasema kwa chinichini kuwa, *"Huyu jamaa anatamani kufa. Jam hana masihara kabisa kwa mwanamke wake kuguswa."*

Minong’ono ya hofu ikanipa uhakika kuwa Jamshid alikuwa kajenga himaya katili ambayo aliiwekea uzio wa hofu kulinda mali zake hadi kuhofiwa hata wakati ambao hayupo. Msichana yule nilipomshika akajinyonganyonga kama nyoka mikononi. Akajitahidi kuniponyoka mara kadhaa akashindwa. Mara ya mwisho alifanikiwa kuniponyoka. Nikaishia kumeza harufu ya manukato yake na kuihisi ngozi yake mororo ikiniliwaza.

Salalee! Kubarikiwa kabarikiwa Jamshid hadi kumiliki wanawake aina ya mrembo yule aliyenipagawisha nikapagawa. Yakawa mapigo ya kuudhoofisha mwili wangu na moyo kwa hisia. Jinsi alinitesa Joyce ndivyo sasa kimwana wa Jamshid alinihenyesha kihisia. Sijui kama nawe utaafikiana nami….lakini itoshe kusema kuwa, ulevi wangu hasa si kilevi cha kwenye chupa, la hasha! Ulevi wangu ni hawa viumbe waitwao wanawake. Kila nikimuona mmoja

ameutekenya moyo wangu huwa najawa ujasiri wa ajabu na kuwa tayari kuua ili niweze kupata uhuru wa kubarizi naye. Hata kama si kubarizi naye sirini kwake, basi nione tu anayofuraha popote atakapokuwa, ila ajue mimi ndiye chanzo cha furaha yake—hilo tu linatosha.

Sasa, kwa jeuri iliyomea nafsini mwangu, na tamaa ya kumchukua kidawa yule, nikauzuia mlango kujifunga ili nibaki namtazama. Akabetua mdomo kama koleo la mchanga kisha akanisonya. Akabofya mahali ili mlango ujifunge kwa nguvu lakini nikatia mguu wangu wenye kiatu kigumu cha jeshi. Aliponitazama mguuni sasa akajua namna buti langu lilikuwa chafu na la aina tofuati kabisa na wastaarabu wa mahali pale. Akaingiwa wasiwasi kuwa huenda nilikuwa haramia ambaye nilitaka kujipatia vijisenti kutoka mahali pale. Ama la, alihisi navizia vito vyake vya dhahabu kwa maana alianza kuficha cheni yake ya

shingoni. Nikaona pia anataka kuvua pete zake na kuzirushia katika chumba kile kigeni kwangu.

"Usinidhuru. Sema nikupe kiasi gani uende!" akasema kimwana yule.

Nilicheka kwa kejeli tu. "Sijaja kukwapua vijihela vya walevi na kahaba hapa." Nikatia tabasamu langu la kejeli tena mbele ya uzuri wake wa asili uliokolezwa na bandia ya kununua. Nikamwambia, "Bwana'ko leo ana mgeni."

Akasonya.

"Mgeni gani?"'

"Naitwa Chato, ukimwambia ataelewa."

Nikautoa mguu wangu na kuuacha mlango ukajifunga. Wakati napiga hatua kurudi mahali nilikuwa, akanisindikiza kwa macho kupitia kitundu kilichokuwa ubavuni mwa mlango. Nilirudi katika meza yangu na kutafakari sana juu ya maisha ya Jamshid. Hakika alikuwa kayakatia bima

maisha kwa kiwango kikubwa sana tofauti na alivyokuwa baada ya kujipatia ngawira katika biashara za ulanguzi na magendo. Nikawaza mahali alizipata pesa sufufu namna ile na nikakumbuka mengi ya ndoto zake. Yeye alikuwa tayari kuua ili amiliki pesa. Alikuwa tayari kufanya haramu ili ajipatie maisha matamu. Sasa wasiwasi wangu ni kuwa, kwa uchu wa pesa na maisha matamu ni lazima alikuwa anafahamu yalipo magenge ya wahalifu. Mara nyingi watu wa Casino kama yeye wanajua mambo mengi ya haramu, na mara kadhaa hushiriki kujipatia mali kwa uharamu.

Basi nikavamiwa na wazo kuwa nimpigie simu Jamshid. Nijitambulishe. Asiponielewa basi nitachukua hatua ya pili kwa kummteka kimwana wake. Lazima Jamshid angenitafuta tuzungumze.

Niliiandika namba ya simu ambayo nilimpigia nayo Jamshid siku nawasafirisha

mke wangu na mtoto. Jamshid hakupatikana. Nikarudia tena na tena, hakupatikana.

Kichwa kikapata babaiko na hasira zikanijaa kifuani. Nikahisi kabisa kuwa Jamshid aliamua kunikwepa. Huenda aliniona akaamua kuondoka na kuizima simu yake ili nisimpate. Kama ndivyo, alikuwa anajidanganya!

Wakati nataka kuelekea alikokuwa kajifungia yule kimwana nikastaajabu sana. Kwa ghafla mno nikaona askari wanne wakiwa wanaingia mahali pale. Nikawaona jinsi walifika kwa shari. Mmoja alikuwa na bastola mkononi. Hapohapo nikarudisha mkono wangu mahali nilihifadhi chuma changu cha kazi—bastola iliyokuwa na uwezo wa kunitii wakati wowote nikitaka ifanye kazi. Ningali nimewakazia macho, nikawaona wanapita na kuelekea kwenye mlango ambao mrembo alijifungia. Bila subira wakauvamia mlango kwa mateke na

kukimwaga kioo chake huku wakifoka ati kwanini wanaendelea na biashara ya Casino kinyume na sharti la kujiepusha na mikusanyiko dhidi ya Korona.

Baada ya muda nikasikia kelele za msichana akilia kwa hofu. Kilio cha mwanamke kwangu huufanya moyo kuzingirwa na ujasiri wa ajabu. Nikaingiwa huruma kuhisi binti yule anadhulumiwa na wanaopaswa kumlinda. Nikatoka mkuku kwenda huko. Nilipochungulia nikawaona wale askari wamemzingira msichana yule. Walimtomasa maungoni na mwingine alikuwa akimtilia kidole sehemu zake za siri. Nikaona namna alihangaika kujitoa mahali pale. Kila alipotakiwa kufanya jambo ili wamwingilie aligoma. Nikashuhudia namna walimpiga makonde ya rasharasha kumtisha na kumchania blauzi iliyositiri matiti yake laini. Nikaona huo ni upuuzi kuuvumilia. Hata kama nipo katika ardhi ya ugenini, lazima niwatetee wanyonge. Hiyo

ndiyo kazi yangu. Nikaamua kununua kesi kwa gharama ama bure.

Nilipofika mlangoni nilijua tu jambo la kwanza wao kulifanya ni kutaka wanikamate ama wanishushie risasi endapo ningetia juhudi kuwakatili wasifanye uhayawani wao. Nikaanza kwa uoga. Nikamtandika risasi mmoja ambaye alikuwa mwanzoni. Risasi ile korofi ikamshona mkononi hadi bastola aliyokuwa nayo ikamponyoka. Mmoja hakuwa na silaha lakini wawili waliobaki nikawachachafya kwani hawakuwa na risasi za kutosha kwenye bastola zao. Walipojibu nilikwepa na nikashuhudia wakibaki midomo wazi baada ya risasi kuwaishia. Niliwachakaza kwa risasi hadi nilipoona wametulia sakafuni.

Sikuwa nimekusudia kuua.

Nilimshika msichana yule na kutoka naye baada ya kusikia kabisa kupitia redio ya upepo kuwa polisi walipata taarifa za

timbwili lile. Tukaelekea penye maegesho huku kila aliyekuwa mahali pale akiwa anajaribu kujiondoa kwa haraka baada ya milio ya risasi. Hata kama palikuwa na msukosuko, huo ndio ulikuwa wakati wa kumgusa kwa hiari yake mrembo yule. Nikavua koti langu lililokuwa na vumbi na majasho ya safari ile ndefu na kumfunika ili asiendelee kubakia kifua wazi. Wakati huu hakuleta ukorofi kwa maana alilainika akakubali kunifuata kila hatua. Mikogo ya kutembea kwa kuchechemea kama mlemavu hakuwa nayo tena. Sasa mguuni hakujali hata kuwa alitembea pekupeku kama bata. Nilichosikia akikisema ni kuwa nimsaidie asidhuriwe. Akanishika kwa nguvu ili nisimponyoke. Alikuwa akitikisika kwa hofu.

Kuna gari moja ilikuwa karibu na pale Jamshid aliegesha gari aliyotoka nayo. Ilikuwa gari aina ya Stela Blue CX. Ni gari nzuri yenye rangi ya dhahabu na mng'aro

wa almasi. Ni gari ya chini wala si ndefu kwenda juu. Pia umbo lake ni la kubadilikabadilika. Ilikuwa na uwezo wa kupungua upana wake mtu akapita kichochoro na kwenda zake. Na kuna wakati ukitaka unaweza kuiachia ikatanuka na kuwa pana. Na wakati ukiona inafaa ilikuwa na nafasi ya kubonyeza tu na kuchagua umbo la ndege ya abiria. Hiyo ndiyo gari iliyokuwa yake manzi wake na Jamshid.

Nilimsukuma msichana yule aingie ndani ya gari lile. Nikatupia macho mahali ninapojua huwa na ufunguo. Wapi! Nikachungulia tena na tena, sikupaona.

Kwa alivyokuwa kababaika nikamsikia msichana yule anasema, "Endesha twendeee!"

Akanipigapiga mgongoni huku anaipigapiga pia miguu yake pale alipokanyaga. Sikuitoa gari mahali pale.

Niligeuka na kutazama sehemu ya ofisi pakiwa panaishilia watu wakikimbia.

Nikamweleza mrembo yule kuwa,“Ufunguo hakuna!” Nilipotamka kuwa hakuna ufunguo ndipo akakumbuka. Nikaona anaingiza mkono katika mfuko wa sketi yake na akatoa kiunga mbali (rimoti) nikabofya tu na kwa haraka gari ikawaka Tukaondoka kwa mwendo mkali huku nasikia kabisa ving’ora vya magari ya polisi eneo hilo.

Barabara niliyoifuata si ya kwenda kwa Jamshid wala mjini kati, bali ni nje ya mji. Nikaongeza kasi na tulipofika sehemu ambayo nilidhani ni salama, niliegesha gari mafichoni—sehemu yenye miti iliyoshusha matawi yake kama jumba. Nikamshika yule msichana na tukaelekea kwenye hoteli ambako ilikuwa si rahisi kufahamika kwa wengi.

Sehemu tuliyoelekea ilikuwa si ya kustarehe watu kama Jamshid na mpenzi

wake. Ni sehemu ya ajabu, kwa mrembo kama yeye lazima angeona ni mahali pachafu na hapafai kwa binadamu kama yeye. Ikawa wakati wa kuniuliza, "Mbona umekuja huku? Hapa.—pachafu hivi"

"Hupaswi kuuliza sana…nyamaza…"

"Wewe nani?" Akauliza tena.

"Umechanganyikiwa? Si nimekueleza naitwa Chato. Umesahau? Kama hujaelewa ngoja utanijua baadaye. Mimi mgeni wa Jamshid."

"Unataka nini sasa?"

"Punguza maswali malaya wewe." Nilifoka na kuunyanyua mkono wangu ulioshiba kwa mazoezi nusura nimzabe kofi. Shabash! Kidomodomo chake kikataka kumponza, ila bahati yake nikajizuia. Nikaona kumpa adhabu ya namna ile ni kumwonea tu kiumbe yule dhaifu. Alishazoea vitu laini. Alichokiona ni mkono wangu ulioshiba misuli ukiishia karibu na shavu lake laini kama nyanya mbivu. Macho

akayatoa na kunistaajabu nilivyokuwa nimekusudia kumpa kichapo.

“Nisamehe!” akasema.

“Nyamaza!” nikamkemea.

Akababakia kimya akinitazama.

Mhudumu wa hoteli tuliyoenda akawa tayari kutuonesha chumba. Kwa hali tuliyoikuta pale chumba kilichokuwepo ni kimoja tu—tena cha kusubiri.

“Tutasubiri kwa muda gani?” niliuliza.

“Kama dakika—ah—tano au sita.” Akajibu.

Kwanza nikacheka utadhani alinitekenya mhudumu yule kwa maneno yale.

“Kwa maana kuna mtu anapaswa atoke ndipo tuingie, au inakuwaje?” nikauliza.

“Walioukuwemo wametoka sasa hivi—nataka nifanye usafi tu,” akajibu. Akaniangalia mara mbilimbili juu hadi chini kisha akamtazama binti yule nilikuwa naye.

“Umeopoa chuma hatari! Ngoja nifanye haraka kiu yako ikatike.”

Sikukasirika ila nilibaki kutabasamu tu bila hata kujali aliyoyasema. Nilichowaza ni kuwa anasafisha na kutupa chumba ambacho tayari kimeshatumika punde tu. Kwa maana kuna mtu alikuwemo na mpenzi wake wakifanya yao, sasa washatoshana ni zamu yetu. Loh! Nikameza funda la mate kisha nikaanza kusogea kando na mlango wa kutokea katika hoteli ile iliyochakaa.

Baada ya kuingia chumbani msichana yule hakuwa na utulivu. Kwanza chumba kile kilikuwa na mwanga hafifu sana. Dari lake lilikuwa na ramani ya mvujo wa maji ya mvua—isitoshe hivyo, lilikuwa limeoza likaning’inia upande na kulisogelea feni lililokuwa likizunguka kivivu likijaribu kuzalisha hewa nzuri na kuitoa hewa ya hovyo iliyojazana katika chumba kile. Kitanda kilichokuwa katika chumba kile

kilikuwa kidogo kiasi kwamba mkilala wawili lazima muwe wapenzi. La sivyo ni dhahama tu. Nikakisogelea na kuketi kama jaribio—kikatoa kelele kama baiskeli iliyoishiwa grisi nywi—nywii. Kikaenda upande huku na kule kikijigonga ukutani.

Yule msichana akatingisha kichwa huku amesimama wima akinitazama kwa hofu.

"Mpigie simu Jamshid," akaniamuru.

Sikumjibu.

Hatimaye mlango ukagongwa. Nikasimama haraka na kwenda mlangoni. Nikaufungua mlango na kukutanisha macho na mhudumu wa ile hoteli.

"Chumba gani hiki umetupatia?" nikamuuliza.

"Mchagua jembe si mkulima—fanya kazi yako manzi afurahi. Kitanda siku hizi ni *old fasheni*. Shika blanketi hili utatandika chini hapo. Hakuna chandarua kwa sababu hapa hamjaja kulala. Najua hapa ni kazi moja tu—

ambayo mbu hawataweza kuwasumbua.” Akatapika maneno msichana yule. Nilimtazama kisha nikalitazama blanketi lake. Lilikuwa safi lakini lilikuwa na harufu ya jiki ingali kali puani.

Nilifunga mlango na kuelekea ndani. Msichana yule hakuketi wala kulala. Alibaki kasimama wima akinitazama kwa hofu. Alidhani sasa kama kubakwa ulikuwa muda maalumu. Hata asingejisumbua kuwaza namna ile. Mimi najijua—siwezi kula nyamafu. Siwezi kujifaidia kisicho hiari na wala siwezi kutumia mkasa kufanya mkasa mwingine. Napenda hiari iamue kama hiari yangu dhidi ya chanjo ya korona.

Nikamtazama. Nikawaza hivi na vile. Nikawa namtazama nakumeza mate tu japo sikutaka kumfanya kitoweo. Wakati huo koti langu alishalitupa kwenye kiti na kajifunika lile blanketi kusitiri kifua chake—kwani alikuwa kachaniwa blauzi na baadhi

ya nguo za kumsitiri na wale polisi wenye inda.

"Pumzika. Mimi nitakuwa wima kukulinda hadi kieleweke. Najua mambo yashakuwa moto sasa—maana polisi niliowaua lazima wenzao watataka kulipa kisasi. Watanisaka kila mahali," nilieleza.

"Sasa si uende uniache!" Akasema.

"Nikuache kwa sababu gani? Mimi sina akili kama huyo Jamshid wako. Inakuwaje nikuache mwanamke mrembo kama wewe halafu uishie kuwa mboga ya wapuuzi wale masikini wanaofugwa kituo cha polisi! Kama ulitaka niondoke, basi ungesema maneno hayo wakati ukiwa pale *Night Club,* wakati wanataka kukusasambua hao wapumbavu."

Akanikazia macho mrembo yule kwa jinsi nilikuwa nimefubaa moyo. Nikakutanisha macho yangu na yake. Akaona aibu kwa kuyashusha chini na kuacha kunitazama maana macho yangu

yalijaa chuki kwa sababu ya hasira. Nikahisi sasa nimemaliza utata wa hisia zake kuwa mimi ni mwanaume wa namna gani. Mwanaume jasiri ni sawa na simba—hapwesi macho kumkwepa mwanamke. Hata wanawake wanajua—ukiona dume linaangalia chini dhidi ya mwanamke jua hapo kuna walakini hata faraghani. Wanawake wanapenda jasiri ambaye anaweza kufanya jambo kwa kujiamini.

"Sikiliza wewe kiumbe…unalo deni kubwa la kulipa."

"Mimi?" akauliza kijinga.

"Sasa unataka awe nani?"

"Deni gani?"

"Utajua nikianza kukudai!"

"Kwanini?"

"Naomba sana upunguze maswali. Mimi sipendi kuulizwa-ulizwa kama mwanafunzi kilaza darasani. Jua mimi nitakudai na kunijibu kwako ni kulipa deni langu."

Akapandisha na kushusha pumzi. Akawa kashikwa na butwaa muda wote. Nikaitafuta namba ya Jamshid tena lakini sikufanikiwa kumpata.

"Una namba ya Jamshid?" Nilimuuliza msichana yule.

"Ndo ulikuwa unanidai hiyo?"

"Acha upuuzi wako, malaya!"

"Malaya nani?"

"Wewe na bwana'ko!"

Akataka kunyanyuka anivae kwa hasira.

"Shhhhh! Tazama hujavaa hata nguo ulipo. Usitake nikajionea sinema ambayo mchezaji wake ni mimi mwenyewe."

Akanywea.

"Nitajie namba!"

Akanitajia.

Nilipopiga nikasikia Jamshid anapokea kwa mahaba. "Naam, Joyce Mpenzi!"

Ha! Nikastaajabu sana. Nikasita kuongea kwani sasa nilibaini Joyce alikuwa anafahamiana na Jamshid na huenda ni kwa sababu ya kuwa ni muuza mafuta na Jamshid mnunuzi wa mafuta kwa ajili ya gari zake. Nikakata simu kwani namba niliyopiga nayo ni ya Joyce.

Nilipachika kadi yangu ya simu haraka na kumpigia Jamshid ambaye naye hakuwa na namba yangu hiyo mpya. Akapokea…

"Polisi wanakutafuta. Kaa chonjo. Mrembo wako ninaye hapa nimemnusuru dhidi ya polisi wale wahalifu. Alimanusura wamsasambue!"

"Unasema nini? Wewe nani? Na huyo mrembo wangu ni nani?" Jamshid akauliza maswali kibao.

Msichana yule akaninong'oneza kuhusu jina lake.

"Mwambie Esta!"

"…mrembo wako anaitwa Esta!"

Jamshid akashtuka.

“Wewe ni nani?”

“Chato!” Nikajitambulisha kwa ukali.

Jamshid nikahisi alijua mambo yameharibika sasa, kwani nilisikia babaiko katika sauti yake.

“Nataka nijue mke wangu na mtoto waliko. Hilo ndilo la muhimu zaidi,” nikafoka. “Kama hunipi jibu la maana hata huyu Malaya wako usitake kujua habari zake.”

Akababakia kimya.

Nikarudia swali langu, tena akababakia kimya.

Nikakata simu.

Baada ya muda mfupi Jamshid akapiga simu.

“Chato…niambie ulipo nije tuzungumze!”

“Wewe niambie familia yangu ilipo, sijaja kuzungumza na mtu aliyeshindwa kuwalinda watu wangu muhimu.”

“Nitakwambia nikija.”

“Basi acha nitajua walipo mwenyewe.”

“Usiwe hivyo Chato. Inasemekana wametekwa na makachero wa huko Tuvumiliane!”

“Ulishindwa kuwalinda?”

“Hapana?”

“Sasa mbona imetokea hivyo? Bila kuwapata nawe sahau kumpata huyu Esta wako. Wakiuawa huyu atakuwa mbadala wao.”

“Sikiliza Chato….sisi ni marafiki na nashukuru umekuja tushirikiane kuwatafuta waliko. Itakuwa rahisi. Kumbuka pia unachofanya katika nchi yetu ni kosa la uhaini. Ukikamatwa adhabu yake ni kifo…”

“Inategemea hicho kifo atakufa nani…wewe au mimi.” Nikakata simu.

Riwaya hii inaendelea hadi mwisho. Ukitaka nakala ngumu weka Oda kwa

1. NAMBA 0743 017 563 (SMS, DIRECT CALL)
2. NAMBA 0625 813537 (WhatsApp)

   Nakala laini kitabu kizima kinapatikana kwa Tsh. 5000/=

   Ukitaka kujiunga na group maalumu la kusoma riwaya zote mpya pamoja na hii unalipa Tsh. 3000/= kwa mwezi. Kutakuwa na riwaya 3 zinazoendelea hadi mwisho. Vigezo na masharti vitazingatiwa kwa wanaojiunga na kundi.

Share sample ya Riwaya hii popote na marafiki..bureeee.

**TAZAMA MACHAPISHO MENGINE KURASA ZIFUATAZO 10,000/@**


MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA
JOHN WISSE
Anayewinda..
anawindwa...mwendo
wa kuwahiana..
KISIRANI
PAKA HAWEZI KUISHI KWA MSELA


MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA
JOHN WISSE
Misheni #5
MOSCOW
Risasi zimeisha, adui wanamwandama kama nyuki...
akikamatwa ni kifo...kilichobaki ni kupigania pumzi....
Raymond Chato sasa yupo shimoni...


MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA
JOHN WISSE
PROPAGANDA
NIUENI MKITAKA, UKWELI WOTE NITASEMA
...shushushu wa taifa anabaini faili lenye siri nzito kuhusu mpango wa chanjo ya Korona. tayari kufa akitetea taifa lisiwekwe rehani. Sasa anahatarisha usalama wa taifa na wake mwenyewe. Atafanya nini wakati anawindwa kuuawa?"


Mwalimu
Msiri
JUA HALIKIMBIWI
JOHN WISSE
MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA


MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA
JOHN WISSE
MISHENI #3
ARUSHA
MUUAJI LAZIMA APATIKANE


....kuanza kutumika kwa sarafu ya kraiptoni (crypto currency) iitwayo Warton, na kukomeshwa kwa sarafu zote duniani kunarejesha utumwa kwa jamii za kiafrika...sasa kufa huku unaishi...
SARAFU
NYEKUNDU
ZUBAA UZIKWE MZIMA
JOHN WISSE
MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA


Kachero wa kukodi, Raymond Chato anapaswa kumwokoa binti wa tajiri wa Kitanzania aliyenaswa katikati ya mapigano mjini Donboss. Je, ataweza wakati eneo lenyewe limejaa uasi na mauaji ya kila mgeni ndani ya mji?
MISHENI #4
UKRAINE
TUMAINI LIPO GIZANI
JOHN WISSE
MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA


(kumbukumbu ya mauaji)
walitaka
GIZA
wakaizima
NURU
John Wisse
MTUNZI #1 WA BETA DAISTOPIA